# MUONGOZO WA HAJJ, UMRAH NA ZIYARAH


**KIMEKUSANYWA NA**

Abul Khatwaab Abdallah Humeid
Al-Hadhramy

**UTANGULIZI**

Abul Fadhil Qaasim Bin Mafuta
Bin Qaasim




بِسْمِ ٱللَّٰهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Ewe Allah Mola wetu! Sifa njema zote ni zako, na shukran zote ni zako. Sifa njema zote ni zako mpaka uridhike na utakaporidhika na baada ya kuridhika.

Swala na salaam nyingi zimfikie mtume wetu Mtukufu Muhammad na Aali zake na maswahaba zake wote na wale walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.

Ama baada ya kumsifia Mola wetu Mtukufu Tabaaraka wa Ta'alaa na kumswalia mjumbe wake mkarimu swalla Ilaahu alayhi wa Aalihi wasallam. Kwa hakika kuna umuhimu mkubwa sana wa kuisahilisha elimu kwa watu hususan katika mambo ya itikadi na ibada, na miongoni mwa ibada ambazo zinawatatiza ni ibada ya Hajji. Watu wengi hujikafilisha kutoa mali zao. Kuwaacha ahli zao na miji yao kwa ajili ya kumuitikia Mola wao Mkarimu katika kuitekeleza ibada hii, lakini kwa masikitiko makubwa si wote wanaoipatia ibada hii, bali wanaokosea ni wengi mno, pamoja na kwamba Maulamaa wa Kiislamu wametoa juhudi kubwa tangu zamani ya kuandika vitabu katika maudhui hizi, lakini tatizo kubwa linalowakabili ndugu zetu wengi ni kutokufahamu lugha ya kisheria, lugha ya Kiarabu, lugha ya Qur-ani na lugha ya Mtume wetu swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam.

Na kwa sababu hiyo ndipo alipojitolea Ndugu yetu kipenzi. **Sheikh Abul-Khatwaab Abdallah Bin Humeid Al-Hadhramiy**-*Allaah amlipe kila la kheri na amuhifadhi na kila la shari*-kuisahilisha ibada hii kwa kuileta kwenye lugha ya Kiswahili. Lugha inayofahamika na watu wengi wanaoishi kwenye mwambao huu wa Africa ya Mashariki, Bara na Visiwa vyake.

Kitabu hiki kimekuwa cha aina ya pekee, kwa kuwa mwandishi ametoa juhudi kubwa ya kuyaweka kila mas-ala na dalili zake. Allaah atupe Tawfiq sisi na yeye katika kuifikia haki na kufanya yale yanayomridhisha Allaah Subhaanahu wa Ta'alaa.

***Abul Fadhil Qaasim Bin Mafuta Bin Qaasim***

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

# HAJJI NA UMRAH

Sifa zote njema ni zake Allaah, aliyesema katika kitabu chake kitakatifu:

"وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ"

**"Na kwa ajili ya Allaah imewajibika watu wahiji kwenye nyumba hiyo (iliyoko Makka), kwa yule awezae njia ya kwenda, na atakaye kanusha basi Allaah si mhitaji kwa walimwengu."**

**(Al Imran aya 97)**

Ama baada ya hayo:

Kwa hakika ibada ya hajji ni katika alama tukufu ya dini hii ya Uislamu, ambayo Allaah Subhaanahu wata'ala ameikokoteza na kuihimiza itekelezwe, na kuweka malipo makubwa kwa yule atakae itekeleza ibada hii tukufu, amesema Mtume ﷺ: **"Hajji iliyotimia haina malipo mbele ya Allaah ila ni pepo."** Na nyenginezo katika dalili zinazo onyesha utukufu wa ibada hii na malipo yake makubwa.

Kwa sababu hiyo na nyinginezo, yampasa Muislamu achunge sana anapoifanya ibada hii tukufu, ajitahidi kwa kadri atakavyoweza kuifanya iwe ibada yake itaambatana na mafunzo ya Mtume ﷺ. Ili kutekeleza amri yake Mtume ﷺ aliposema: **" chukueni kwangu matendo yenu ya hajji."**

## Ili Ibada Yako Ya Hajji Itimie, Zingatia Yafuatayo:

1. Jiepushe na SHIRKI na UZUSHI katika dini, kwa sababu shirki ni yenye kuondoa na kuharibu amali zote!! Kama alivyosema Allaah:

" وَلَقَدْ أُوحِيَ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكَ لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ"

**"Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa waliokuwa kabla yako: bila shaka ukimshirikisha Allaah a'amal zako zitabatilika na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasirika."**

**(Azzumar aya 65.)**

2. Tubia kwa Allaah kutokana na madhambi yako yote, ili ikubaliwe hajji yako na umra, kwa hakika Allaah amesema: "إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ اللَّهُ مِنَ الْمُتَّقِينَ"

**"Allaah huwapokelea** wenye kumcha **." (Al maaida aya. 27.)**

3. Jiandae na safari yako ya ibada hii na mali ya halali, na ujisafishe kutokana na mali ya haramu ili ukubaliwe maombi yako.

4. Kuwa na ikhlaas katika nia yako, wala usikusudie katika hajji yako au umra kujionyesha wala kutaka kusikika. Na lau kama mtu atafanya biashara haitaathiri kuswihi hajji yake kama wanavyodhani watu wengine.

5. Jifunze hukmu za hajji na umra na hukmu za safari kama kupunguza na kuunganisha swala n.k, na uulize kila kinacho kutatiza katika ibada yako, na ni bora kuwa na kitabu kizuri kitakacho kupa muongozo katika ibada yako.

6. Kutowaudhi waumini wenzako kwa mijadala mengi ya baatil, Allaah amesema katika kitabu chake: "فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ الْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي الْحَجِّ"

**"Na anaye kusudia kufanya hajji katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu, wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika hajji." (Al baqara aya.197.)**

## Ni nini hukmu ya Ibada ya Hajji?

Allaah Subhaanahu wataala anasema: **"Na kwa ajili ya Allaah imewajibika watu wahiji kwenye nyumba hiyo (iliyoko Makka), kwa yule awezae njia ya kwenda, na atakaye kanusha basi Allaah si mhitaji kwa walimwengu." (Al imran aya. 97.)**

" وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۚ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ "

Kwa hiyo hajji ni nguzo katika nguzo za Uislamu, kwa ushahidi wa maneno ya Mtume ﷺ : "Uislamu umejengwa na nguzo tano...akataja: Kuhiji nyumba ya Allaah (iliyoko Makka)".

Na ibada ya hajji ni wajib katika umri wa Muislamu mara moja.
Ni wajib kwa Muislamu akimbilie kuitekeleza ibada hii pindi tu anapopata uwezo, kwa kuchelea mauti yampate kabla hajaitekeleza!

## Sharti za kumwajibikia mtu Ibada ya Hajji

1. Uislamu, kwa hiyo hajji sio wajib kwa asiyekuwa Muislamu, bali haijuzu kwake kuingia mji wa Makka, ataamrishwa asilimu ndipo aruhusiwe kuingia Makka.

2. Akili timamu, kwa hiyo hajji sio wajib kwa mwendawazimu wala haisihi hata akifanya kwa kukosekana sharti la akili timamu.

3. Kubaleghe, kwa hiyo sio wajib kwa ambaye hajabaleghe, ingawa akiifanya itaswihi na atapata ajri yule anaempeleka, ila tu anapobaleghe inampasa afanye hajji yake tena.

4. Awe huru wala sio mtumwa.

5. Kuwa na uwezo wa kimali na kimwili, awe na uwezo wa kimali katika safari yake hiyo, na awatosheleze atakao waacha nyuma ambao ni jukumu lake kuwasimamia kimahitaji.

## AINA YA IBADA YA HAJJI

**1. Tamatuu"**: Nayo ni ahirimie katika miezi ya hajji kufanya umra pekee, anapofika Makka hutufu na kufanya Sa'ayi kisha hunyoa nywele, inapofika siku ya Tarwiya (tarehe nane Dhul Hijja) huhirimia kwa ajili ya hajji pekee na hufanya yote yanayo mpasa kufanya aliye katika hajji.

**2. Qiraan**: Nayo ni ahirimie hajji na umra pamoja, anapofika Makka hutufu twawaaful quduum, kisha afanye Sa'ayi baina ya Swafaa na Marwa kwa ajili ya hajji na umra pamoja, kisha atabaki katika ihram mpaka siku ya Idd ndipo atakapo halalika.

**3. Ifraad**: Nayo ni ahirimie kwa ajili ya hajji peke yake, anapofika Makka hutufu twawaaful quduum, kisha hufanya Sa'ayi ya hajji yake, atabaki katika ihraam mpaka ahalalike siku ya Idd, na hachinji.

# MIIQAAT

Mtume Muhammad ﷺ aliweka miiqaat ambayo ni mipaka inayo anziwa ibada ya hajji ama umra, ni wajib kwa kila anayetaka kufanya hajji ama umra kuhirimia kuanzia hapo.

### Miiqaat yenyewe ni kama yafuatayo:

- Miiqaat ya watu wa madina na wanaopitia madina ni Dhul Huleifa, hujulikana leo kama Abyaar Ali, umbali wake na mji wa Makka ni 450km.
- Miiqaat ya watu wa Sham, Misr na Morocco na wale wanaopitia njia yao ni Juhfa,iliopo karibu na mji wa Raabigh, na watu huhirimia leo kutoka Raabigh, umbali wake na mji wa Makka ni 183km.
- Miiqaat ya watu wa Najdi na wale wanaopitia huko ni Qarnul manaazil, na leo huitwa Asseilul kabiir, umbali wake na mji wa Makka ni 75km.
- Miiqaat ya watu wa Yaman na wanaopitia huko ni Yalamlam, na leo watu huhirimia sehemu inaitwa Sa'adiyya, umbali wake na mji wa Makka ni 92km.
- Miiqaat ya watu wa Iraaq na wanaopitia huko ni Dhaatu I'rqi, umbali wake na mji wa Makka ni 94km.

Ni wajib kwa kila anaepitia hizi miiqaat akiwa na niya ya kufanya hajji ama umra ahirimie kutoka hapo, iwapo ataipita miiqaat bila ya kuhirimia, hakuna budi atalazimika kurudi tena ili ahirimie katika miiqaat, na iwapo hatarudi, akahirimia baada ya kuipita miiqaat basi atalazimika kuchinja.

**Zindusho:** Jidda sio miiqaat kwa wale wanaokuja kutoka nje, ingawa watu wa Jidda huhirimia hapo, kwa hiyo jichunge usije ukaifanya Jidda ni miiqaat!!



**Matendo Ya Anayetaka Kufanya Umra au Hajji Katika Miiqaat**

1. Inapendekezwa aoge kwa ajili ya ihram, hata akiwa ni mwanamke aliye katika ada ya mwezi au damu ya uzazi.

2. Ni Sunna kujipaka manukato mazuri yenye harufu nzuri mwilini, katika ndevu na nywele kwa waume, pasi na nguo ya ihram, ama wanawake yasiwe na harufu inayojitokeza, na hapa ni kabla ya kuhirimia, ama baada ya kuhirimia ni haram.

3. Atanyoa na kuondoa kila alicho ruhusiwa kukikata, kama sharubu na kusafisha sehemu za siri na kila anacho hitajika kukiondoa katika mwili wake, na kitendo hiki hakihusu ihram ila ni kwa sababu asije akahitaji kujisafisha baada ya ihram na hapo itakuwa ni haramu kwake, ama ndevu ni haramu kunyoa kabla na baada ya ihram, bali katika nyakati zote ni haram kunyoa!!

4. Kisha kwa mume atavaa izari na ridaa, yapendekezwa zaidi ziwe nyeupe tena safi, ingawa sio sharti bali yajuzu kuvaa rangi nyingine yeyote. Ama mwanamke anaruhusa kuvaa nguo yeyote aliyozoea, kwa sharti asijifananishe katika vazi lake na wanaume wala lisiwe vazi la kuwavutia wanaume ikawa ni fitna! Ama kukhusisha vazi la mwanamke kuwa rangi nyeupe au kijani, ni katika mambo ya uzushi yasiyo na mashiko yoyote katika dini.

5. Yajuzu kwa muhrim kuvaa ihram yake kutoka nyumbani kwake, kama alivyofanya Mtume ﷺ na maswahaba wake, hili humfanyia wepesi zaidi yule anaye safiri kwa ndege, kwa sababu ni uzito kuvaa akiwa juu ya ndege, kwa hiyo itajuzu kwao kupanda ndege wakiwa na vazi la ihram, lakini hawatahirimia hadi wakaribie au wafike katika miiqaat.

6. Ihram haina swala maalum, ila ikisadifiana na swala basi ataswali swala yake ya faradhi kisha aingie katika ihram, ikiwa sio wakati wa swala ya faradhi basi ataswali rakaa mbili kwa niya ya Sunna ya wudhuu, kwa mwanamke aliye katika ada ya mwezi au damu ya nifas basi hana swala.

7. Baada ya kumaliza kuswali atahirimia (na hii ni kwa wale walio katika miiqaat), na ihram ni niya ya kuanza matendo ya hajji au umra, atanuwiya kwa moyo wake aina ya hajji anayotaka kuitekeleza au atanuwiya umra ikiwa ni umra, na hapa atatamka kile alicho kinuwiya, ikiwa ni tamatuu' atasema:

لبيك اللهم بعمرة
***Labaika llahumma bi umra.***

8. Kuanzia hapo atakuwa ameingia katika ibada yake, hapo ataanza kuleta talbiya, nayo ni kama ifuatavyo...

" لَبَّيْكَ اللَّهُمَ لَبَّيْك،لَبَّيْكَ لاَ شَرِيْكَ لَكَ لَبَّيْك،إِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لكَ وَالْمُلْك لاَ شَرِيْكَ لَكَ "

***"Labeika llahumma labeik, labeika laa shariika laka labeik, innal hamda wanneemata laka wal mulk laa shariika lak."***

9. Anaamrishwa anayeleta talbiya awe atanyanyua sauti yake, kwa sababu ndivyo alivyo amrisha Mtume ﷺ .

10. Wanawake pia ni kama waume katika hili, watanyanyua sauti zao maadamu hakuogopewi fitna, ama wakiwa karibu na waume watashusha sauti zao.

11. Atalazimiana na talbiya njia yake yote, kwa sababu ni katika alama kubwa za hajji.

12. Atakapo fika mji wa Makka akiona majumba ya Makka hapo ataikata talbiya ili kujishughulisha na yanayofuata katika ibada.

## Mambo ambayo sio makosa kwa Muhrim (Aliye katika Hajji au Umrah) Kuyafanya

Ni jambo la muhimu kwa kila mlinganizi, awe atalazimiana na kuwafanyia watu wepesi katika ibada zao kwa ujumla, na mahujaji khaaswa, kwa sababu wepesi na usahali ni katika misingi ya sharia yetu ya Kiislamu tukufu, kama inavyo julikana, maadamu wepesi huo hautakhalifu Quran wala Sunna, ama inapokuja dalili basi hapo hamuna nafasi ya kutumia rai wala fikra ya mtu.

Na huu ndio msimamo wa katikati ambao ni wajibu kwa mlinganizi kushikamana nao, wala asizingatie baada ya hapo atakaye sema ametupa mipaka au amezembea, maadamu yupo na msimamo huu mzuri.

Yanayo fuata ni mambo yanayo juzu kwa muhrim kuyafanya ingawa wengi katika mahujaji huyaona ni makosa, kwa sababu ya fatwa zinazotolewa na wale wasio shikamana na msingi tulio utaja hapo juu, nimeonelea nitanabahishe na kuyataja mambo hayo:

1. Kuoga kwa muhrim hata akisugua kichwa chake, hilo limethubutu kwa Mtume ﷺ katika Bukhari na Muslim, katika hadithi ya Abi Ayub radhi za Allaah ziwe juu yake.

2. Kujikuna kichwa hata zikianguka baadhi ya nywele, kwa ushahidi wa hadithi ya Abi Ayub tulioitaja mbele na hili ndilo chaguo la sheikhul islaam -Allaah amrehemu.

3. Kunusa harufu nzuri, kama waridi n.k na kutoa kucha iliyo vunjika.

4. Kujifunika na kivuli cha mwavuli, hema au ndani ya gari, ama kile kinachofanywa na baadhi ya pote la uzushi, kuondoa sakafu ya gari...ni kufanya uzito usiokuwa na faida yoyote!

5. Kuvaa ukanda kiunoni, kuvaa pete pia, yote haya hayakukatazwa, pia kuvaa miwani iwe ni ya jua au ya macho, kuvaa saa ya mkono, kubeba kipochi cha vitu vyako muhimu shingoni.

6. Kuoga kwa kutumia sabuni yenye harufu, kwa sababu si manukato wala haambiwi anaetumia amejipaka manukato, na asipotumia ni bora.

7. Kuuwa wanyama na wadudu wenye kumuudhi mwanadamu kama panya n.k.

8. Yajuzu kwa mwanamke kutumia tembe za kuzuia ada yake ya mwezi, katika hajji na umra ikiwa hazitamletea madhara.

9. Yajuzu kwa mwanamke muhrima (aliye katika hajji au umrah) kusoma Quran hata katika ada yake ya mwezi, na hii ndio kauli ya sheikh Bin Baaz na sheikh Albany Allaah awarehemu.

10 . Yajuzu kwa mwanamke kuhirimia hata akiwa amevaa dhahabu mkononi.

Yote haya yanaingia katika ule msingi tulioutaja juu, ni katika wepesi na usahali wa dini yetu, Alhamdulillah.

## Aliyo haramishiwa Muhrim

Baada ya kuhirimia kutoka katika miiqaat ni haram kwa muhrim mambo yafuatayo:

1. Kupunguza sehemu ya nywele au kukata kucha, ingawa nywele zikianguka au kucha bila kukusudia au akatoa sehemu katika nywele au kucha kwa kusahau, haina neno.

2. Haijuzu kwa muhrim kujitia manukato katika nguo wala mwili wake, ama athari Iliyobakia ya manukato aliyojiweka kabla ya ihram, athari hiyo haidhuru.

3. Haijuzu kwa muhrim mwanamume kujifunika kichwa kwa kinachoshika kichwa, kama kutumia ihram yake, kofia, kilemba n.k. Akifinika kichwa chake kwa kusahau basi anapo kumbuka atoe kilicho kichwani na haimdhuru ibada yake. Ama kwa wanawake katika hali ya ihram ameamrishwa kuwacha uso wazi, lakini akiwa mbele ya waume atajistiri uso wake na viganja vyake kwa kutumia jilbaab yake ili asionekane na waume.

4. Haijuzu kwa mwanamume kuvaa nguo zilizo shoneshwa kwa kadri ya viungo (makhiit), nazo ni nguo zinazo valiwa kawaida k.m kanzu, suruale n.k.

5. Ni haram kuwinda mnyama au kusababisha kuwindwa mnyama au pia kusaidia kuwinda mnyama kwa kuonyesha alipo n.k.

6. Ni haramu kwa muhrim kuoa akiwa katika hali ya ihram pia kumuozesha aliye na mamlaka ya kumuozesha kama binti yake, na kuposa pia haruhusiwi.

7. Ni haram pia kumwingilia mkewe kabla ya kuhalalika, na akifanya kitendo cha ndoa kabla ya kuhalalika, hajji yake itabatilika na atalazimika kuitimiza mpaka mwisho na itambidi arudi tena mwaka mwengine kufanya hajji na pia atatoa fidya, kuchinja ngamia au n'gombe yeye na mkewe, na ni waajib watubie kutokana na dhambi hiyo! Ama ikiwa kitendo cha ndoa alifanya baada ya kuhalalika kwa kwanza (baada ya kutupa vijiwe katika Jamratul 'aqaba na kunyoa, kabla ya twawaaful ifaadha) hapo hajji yake ni sahihi na ni juu yake kuchinja.

8. Ni haramu pia kumkaribia mkewe kwa vitangulizi vya ndoa kama kumbusu n.k.

## NAMNA YA KUFANYA UMRAH

**Twawaaf Ya Umrah**

1. Anapofika mji mtukufu wa Makka yule anaetekeleza umra; inapendekezwa aoge mara tu anapofika mji huo mtukufu, baada ya hapo aelekee masjidil haram kulipo nyumba kongwe ya Allaah, ili kutekeleza matendo yake ya umra, na iwepo atakwenda bila kuoga basi hamna makosa.

2. Anapotaka kuingia msikiti huo mtukufu, atatanguliza mguu wake wa kulia na kusema:

"أَعُوذُ بِاللهِ العَظِيْمِ وَوَجْهِهِ الكَرِيْمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ،اللَّهُمَ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِك"

***"Audhubillahil adhiim wawajhihil kariim Mina sheitwaani rajiim, Allaahumma ftahlii abwaaba rahmatik"***

Na dua hii ndiyo dua ya kuingia msikiti wowote mwengine.

3. Baada ya hapo, ataelekea kwenye Al Kaaba tukufu ili kuanza twawaaf, ni katika Sunna kwa waume kuweka bega la kulia wazi, katika twawaaf ya umra na twawaaful Quduum peke yake.

4. Kisha ataanza kutufu mara saba, akianzia katika Hajarul aswad, akiweza kulifikia Hajarul aswad atalibusu bila ya kuleta msongamano wala kuwaudhi waislamu wenzake kwa matusi, kupigana au kuwasukuma, yote haya si sawa, ikiwa hakuweza kufikia Hajarul aswad, atanyosha mkono na kuleta takbira " الله أكبر " **"Allaahu Akbar"** bila ya kusimama hapo.

5. Ataendelea hivyo katika twawaaf zote saba, kila anapofika Hajarul aswad ataleta takbira, na ana uhuru wa kumtaja Allaah Subhaanahu wataala kwa kila dhikr kama kusoma Quran katika twawaaf na kuomba dua n.k. na ajiepushe sana na kuudhi watu.

6. Anapofika katika nguzo ya Yamaany (nayo ni ile nguzo kabla ya nguzo ya Hajarul aswad) ataishika nguzo hiyo kwa mkono wa kulia ikiwa ataweza kufika hapo, wala hataibusu wala kujipangusa mwili anapoishika kama wanavyofanya wengi wasiojua, akikhalifu kwa kufanya hivyo Sunna ya Mtume swallallaahu aleihi wa sallam, ikiwa hatoweza kufikia nguzo hiyo, basi atapita bila kuishiria kwa mkono wake, pia ni katika Sunna anapofika hapo alete dua hii

«رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَاعَذَابَ النَّار»

**"Rabbanaa aatinaa fi dunyaa hasanatan wafil aakhirati hasanatan waqinaa adhaaba nnaar"**

7. Ataendelea hivyo katika twawaaf yake, akianza katika Hajarul aswad, akimalizia kila mzunguko hapo, hadi mwisho wa mzunguko wa saba, na ni Sunna kwa waume kuharakisha kidogo katika mizunguko mitatu ya kuanzia twawaaf ya umra na twawaaful quduum peke yake.

8. Ahakikishe anayetufu awe katika hali ya twahara kutokana na hadathi kubwa na ndogo, lau mwanamume atamgusa mwanamke basi wudhu wake hautanguki kama wanavyodhani baadhi ya watu, na hii ndio kauli yenye nguvu katika kauli za wanavyuoni, ingawa ni haram kukusudia kumgusa mwanamke ajnabiya.



## Baadhi Ya Makosa Yanayofanyika Katika Twawaaf:

1) Baadhi ya watu hutufu wakapitia ndani ya Al-hijr (ule ukuta mfupi ulioko mbele ya Kaaba) wakiitakidi kuswihi twawaafu yao, na ukweli ni kuwa Al-hijr ni katika Kaaba na ni lazima upitie nje yake ili uwe umetufu.

2) Kushika kila nguzo ya Kaaba, wengine na kuta za Kaaba, wengine na kitambara cha Kaaba na mlango pia, wengine hushika Maqaamu Ibrahim... na haya yote ni uzushi usiokuwa na msingi wowote katika dini, kwa wanawake zaidi hutunga mambo ya ajabu wakaambizana bila kuuliza ukweli wa hayo, ukapata wengi hupata taabu na dhambi juu, kwa kufanya mambo haya ya uzushi.

3) Msongamano wa wanaume kwa wanawake katika twawaaf, katika Hajarul aswad na katika maqaamu Ibrahim kwa hiyo ni waajib kujiepusha na misongamano hayo.

4) Katika makosa yanayo fanywa kutangulia mmoja mbele na kupiga fujo na wengine kuitika kwa fujo katika adhkaar kama hizo, huku ni kuwaudhi waislamu.

## Anapomaliza Twawaaf Atafanya Yafuatayo

1) Kufunika bega lake la kulia.

2) Kuswali rakaa mbili nyuma ya maqaamu Ibrahim akiweza hivyo, la hakuweza basi ataswali sehemu yoyote katika msikiti wa haram, na hii ni Sunna iliyotiliwa mkazo, atasoma katika rakaa ya kwanza suuratul Faatiha na suraatul Kaafiruun, rakaa ya pili atasoma Faatiha na suuratul Ikhlaas, na akisoma sura nyingine mbali na hizi baada ya Faatiha haidhuru.

3) Anapomaliza kuswali ataenda katika zamzam, anywe maji ya zamzam na kujimwagia kichwani, kwani hivyo ndivyo alivyo fanya Mtume ﷺ

## Baada Ya Kumaliza Twawaaf

1. Atatoka mu'utamir (anayefanya umra) kuelekea Swafaa ili kutekeleza Sa'ayi mara saba, akikaribia Swafaa ataanza kwa kile alichoanza kukitaja Allah katika kitabu chake nayo ni Swafaa, atakapo karibia Swafaa atasoma:

«إِنَّ الصَّفَا وَالمَروَة مِن شَعِائر الله»

**"Inna Swafaa wal Marwata min shaarillah"**

2. Hapo atapanda Swafaa na kusimama juu yake, ataelekea Al Kaaba, na kupiga takbira mara tatu, ataomba na kukithirisha dua akiwa amenyanyua mikono yake, atasema:

اللهُ أَكْبَر ،اللهُ أَكْبَر ،اللهُ أَكْبَر ،لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَه،
لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ،يُحْيِي وَيُمِيْتُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْر،
لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَهُ،أَنْجَزَ وَعْدَهُ وَنَصَرَ عبْدهُ وَهَزَمَ الأَحْزَابَ وَحْدَهُ

**Allaahu akbar, Allaahu akbar, Allaahu akbar, laa ilaha illa llah wahdahu laa shariika lahu, lahul mulku walahul hamd, yuhyii wayumiitu, wahuwa alaa kulli shey-in qadiir, Laa ilaaha illa llah wahdahu laa shariika lahu, anjaza wa'adahu, wanaswara a'bdahu, wahazamal ahzaaba wahdahu.**

1. Ataleta hii dhikr mara tatu, baina ya moja na nyengine ataomba dua, kwa hivyo dua itakuwa baina ya dhikr ya kwanza na ya pili, akishaisoma ya tatu atashuka bila kuomba dua.

2. Mikono atainyanyua wakati wa dua pekee, ama wakati anapotaja hii dhikr hatainua mikono.

3. Baada ya kumaliza atashuka aelekee Marwa, atatembea akiomba dua anayotaka, atajiombea nafsi yake, jamaa zake na waislamu kwa jumla, atakapofika katika sehemu iliyo na alama (taa) za kijani, hapo kwa waume watakimbia mbio sana, mpaka afike mwisho wa alama ile ya kijani, ataendelea kutembea tena kama alivyoanza mwanzo hadi afike Marwa.

4. Anapofika Marwa, ataelekea al Kaaba, na atasema yale aliyoyasema akiwa Swafaa bila kusoma aya aliyoisoma mwanzo, na ataomba dua pia kama alivyofanya akiwa Swafaa, akimaliza atashuka ili kurudi tena Swafaa, atatembea hadi atapofika katika alama ya kijani atakimbia hadi afike mwisho wa alama ya kijani, kisha atakamilisha kutembea mpaka Swafaa.

Hivyo hivyo atakamilisha Sa'ayi yake mara saba, kutoka Swafaa hadi Marwa ni mzunguko mmoja, kurudi kutoka Marwa hadi Swafaa ni mzunguko wa pili, ataendelea mpaka amalizie Marwa...

· Si vibaya akiwa amechoka ama afya yake haimruhusu kutembea masafa hayo, apande kigari asukumwe.

· Kwa mwanamke mwenye ada yake ya mwezi, pia aweza kufanya Sa'ayi.



## Makosa yanayo fanywa katika Sa'ayi

1) Wengine wanapoleta takbira hunyanyua mikono kama wanavyo nyanyua katika swala, hapa ni ima mtu afuate Sunna ya Mtume ﷺ ikiwa atapata nafasi ya kuifanya, au awache kufanya lakini asizue jambo ambalo halikuamrishwa na sharia.

2) Wengine hukimbia kuanzia Swafaa hadi Marwa, na usawa ni kama tulivyo eleza juu.

3) Baadhi ya wanawake hukimbia kama waume baina ya alama za kijani, na usawa hili jambo ni kwa waume pasi na wanawake.

4) Katika makosa pia kusoma aya katika kila mzunguko, na usawa ni kuisoma mwanzo pekee.

5) Katika makosa baadhi ya watu hukhusisha kila mzunguko na dua yake khaaswa, na hili pia ni katika kamusi ya uzushi usio na msingi wowote.

6) Kinacho pendekezwa katika Sa'ayi ni kukithirisha kumtaja Allah Subhaanahu wataaala, ingawa wapo wanao nyanyua sauti zao sana, na hili ni kosa, kwa sababu ni kuwaudhi waislamu wenziwe.

## Baada ya kukamilisha Sa'ayi:

Atapunguza nywele au atazinyoa zote (kipara) na kuzinyoa zote ni bora, isipokuwa ukiwa wakati wa hajji umekaribia, basi atapunguza nywele, na ni lazima kueneza kichwa kizima kupunguza au kunyoa wala sio baadhi ya sehemu za kichwa kama wanavyo fanya wengine, ama kwa mwanamke ni kupunguza kiasi ya ncha ya kidole.

Kwa kufanya hivyo atakuwa amemaliza kutekeleza umra yake inavyo paswa kutekelezwa, na hapa yote aliyo haramishiwa kwa ajili ya ihram yatakuwa ni halali, isipokuwa akiwa ni mwenye kufanya hajji ya qiraan ama ifraad, basi hapo atabaki katika ihram.

**TANABHI:**

*Adhkaar zote na dua zote katika twawaaf na Sa'ayi ni Sunna zinazo pendekezwa wala sio waajib.*

# NAMNA YA KUTEKELEZA HAJJI




## Kutangaza Hajji siku ya Tarwiya (Tarehe nane Dhul Hijja)

Siku ya tarwiya ambayo ni siku ya nane ya dhul hijja, matendo ya siku hii ni kama yafuatavyo:

1. Yapendekezwa afanye katika kuhirimia hajji yale aliyoyafanya alivyohirimia umra, katika kuoga, kutia manukato na mengineyo, kisha anuwiye hajji na kuhirimia kwa kusema: **"لبيك حجا"** "Labbaika hajja"

2. Kisha atakithirisha talbiya kwa sauti, ili kudhihirisha Sunna na kutafuta ajri kubwa mbele ya Allah, hili litaendelea mpaka atakapo tupa vijiwe katika Jamratul aqaba.

3. Kisha ataelekea Mina kabla ya zawaal (dhuhri) mchana wa tarehe nane, na ataswali Mina swala ya adhuhuri, alasiri, magharibi, ishaa na alfajiri, na inapendekezwa kulala Mina wala sio wajib kulala Mina usiku wa kuamkia tarehe tisa.

Sunna katika swala hizi atakazo swali Mina awe ataziswali kwa wakati wake, atazipunguza ingawa hata zijumuisha, isipokuwa swala ya magharibi na alfajiri hazipunguzwi.

## Kuelekea A'rafa

Anasema Allaah Subhaanahu wataala:

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَن تَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ ۚ فَإِذَا أَفَضْتُم مِّنْ عَرَفَاتٍ فَاذْكُرُوا اللَّهَ
عِندَ الْمَشْعَرِ الْحَرَامِ ۖ وَاذْكُرُوهُ كَمَا هَدَاكُمْ وَإِن كُنتُم مِّن قَبْلِهِ لَمِنَ الضَّالِّينَ
ثُمَّ أَفِيضُوا مِنْ حَيْثُ أَفَاضَ النَّاسُ وَاسْتَغْفِرُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

***"Si vibaya kwenu kuitafuta fadhila ya Mola wenu Mlezi, na mtakapo miminika kutoka A'rafaat mtajeni Allaah penye Masha'ril Haram, na mkumbukeni kama alivyo kuongoeni, ijapokuwa zamani mlikuwa miongoni mwa waliopotea.kisha miminikeni kutoka pale wanapo miminika watu, na muombeni Allaah msamaha, hakika Allaah ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu." ( Baqara aya 198-199)***

Na akasema Mtume ﷺ: **"Hajji ni A'rafa"**

## Sunna siku ya A'rafa (Tarehe tisa Dhul Hijja) baada ya kuswali fajri Mina:

1. Aelekee A'rafa baada ya kuchomoza kwa jua siku ya A'rafa, hii ni Sunna, ikiwa ataelekea kabla ya kuchomoza kwa jua hamna makosa.

2. Ataleta talbiya au takbira, walikuwa maswahaba wakitoka Mina kuelekea A'rafa pamoja na Mtume ﷺ kuna wanaoleta takbira hawakukatazwa, na kuna wanaoleta talbiya hawakatazwi.

3. Ataswali dhuhri na asri kwa kuzipunguza (rakaa mbili), katika wakati wa mwanzo (dhuhri), kwa adhana moja na iqama mbili, wala hamna swala ya Sunna baina yake.

## Kusimama A'rafa

**Baada ya kuswali (dhuhri na asri):**

1. Atasimama katika mawe yaliyo chini ya jabal Rahma ikiwa sio takliif kwake, la sivyo, Mtume swallallaahu aleihi wa sallam amesema: "Nimesimama hapa na A'rafa yote ni sehemu ya kusimamia."

2. Yapendekezwa kuelekea qibla wakati huo huo ukiwa umelekea Jabal Rahma ikiwa itawezekana, isipo wezekana basi ataelekea qibla hata ikibidi jabal Rahma kuwa nyuma yake.

3. Atanyanyua mikono yake na kuomba kwa unyenyekevu, na ikileta talbiya pia na kusoma Quran ni vizuri.

4. Na inapendekezwa zaidi kukithirisha tahliil kwani ni bora wa kilicho semwa siku ya A'rafa, tahliil yenyewe ni kama ifuatavyo:

« لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيْكَ لَه، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ،يُحْيِي وَيُمِيْتُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْر »

**Lailaha IllaLLah wahdahu la sharikalahu lahulmulku walahul hamdu wahuwa ala kulli shay'in qadir**

5. Ni Sunna kwa aliye simama A'rafa, asifunge siku hiyo, kwa kumuiga Mtume ﷺ

6. Ataendelea katika hali yake hii: kumtaja Allaah, kuleta talbiya, kuomba dua akitarajia kwa Mola wake amjaaliye katika wale atakao waachilia huru na moto.

7. Litakapo tua jua, ataondoka na kuelekea Muzdalifa kwa utulivu na unyenyekevu, nakukithirisha talbiya.

8. Wala haijuzu kuondoka A'rafa kabla ya kutua kwa jua, kwa sababu Mtume alisimama A'rafa hadi lilipotua jua.

## Makosa Yanayo Fanywa Na Baadhi Ya Watu A'rafa

1) Wengine hushukia nje ya mpaka wa A'rafa, na kubaki sehemu hizo mpaka kutua kwa jua! Na hili ni kosa kubwa mno, kwani anaefanya hivyo hana hajji.

2) Wengine huondoka A'rafa kabla ya kutua kwa jua, na hili ni kinyume na Sunna ya Mtume ﷺ kwani yeye alisimama hadi lilipotua jua, napia kwa sababu kuondoka kabla ya kutua kwa jua ni katika vitendo vya jahiliya.

3) Kujikalifisha baadhi ya watu kupanda juu ya jabal Rahma, na kujikalifisha huku hakuna dalili bali ni uzushi katika dini, kama walivyo tanabahisha wanavyuoni.

4) Kuelekea jabal Rahma wakati wa dua na kutoelekea qibla, na hii ni kinyume na Sunna.

5) Kuswali Sunna baina ya swala ya adhuhuri na alasiri, kwani Mtume ﷺ hakufanya hivyo.

## Kulala Muzdalifa

Baada ya kutua jua siku ya A'rafa, ataelekea Muzdalifa, huko atafanya yafuatayo:
**1.** Anapofika Muzdalifa wakati wa swala ya magharibi au ishaa, ataswali swala hizo mbili kwa kuzijumuisha na kuzipunguza (swala ya magharibi itabaki tatu) kwa adhana moja na iqama mbili, wala hataswali baina yake swala ya Sunna, akiogopea kutofika Muzdalifa kabla ya nusu ya usiku ataswali swala hizo njiani, kwa kuchelewa kupita nusu ya usiku kabla ya kuswali swala hizo.

**2.** Na atalala Muzdalifa, na kulala kwake Muzdalifa ni wajib, na Sunna ni alale baada ya kuswali, wala asijishughulishe na kuokota vijiwe, kwani Mtume ﷺ aliswali magharibi na isha kisha akalala, wala hakuamrisha kuokotwe vijiwe isipokua baada ya kuondoka Muzdalifa, na inajuzu kuokota vijiwe hata Mina.

**3.** Wala sio Sunna kuosha vijiwe hivyo.

**4.** Yajuzu wanawake kuondoka Muzdalifa baada ya nusu ya usiku, kadhalika madhaifu kama watu wazima na watoto, kadhalika anaye kuwa pamoja na wao katika wenye nguvu zao.

**5.** Sunna ni kulala Muzdalifa usiku huo mpaka alfajiri, na waswali alfajiri Muzdalifa.

**6.** Baada ya kuswali alfajiri Muzdalifa, inapendekezwa kusimama katika masha'ril haram (*nalo ni jabali lilioko Muzdalifa*) au kusimama sehemu yoyote ya Muzdalifa, ataelekea qibla na kukithirisha kumtaja Allaah, na kuomba dua kwa wingi.

**7.** Baada ya hapo ataondoka kabla ya kuchomoza kwa jua, na njiani ataokota vijiwe saba, ukubwa wa tembe ya maharagwe, ili kutupa vijiwe hivyo katika Jamaratul Aqaba, na vijiwe vilivyobakia atachukulia Mina.

**8.** Ataelekea Mina kwa utulivu na unyenyekevu huku akileta talbiya.

" لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْك،لَبَّيْكَ لاَ شَرِيْكَ لَكَ لَبَّيْك،إِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لكَ وَالْمُلْك لاَ شَرِيْكَ لَكَ "

***"Labeika llahumma labeik, labeika laa shariika laka labeik, innal hamda wanneemata laka wal mulk laa shariika lak."***

## Matendo Ya Siku Ya Idd (Tarehe Kumi Dhul Hijja)

Matendo ya hajji katika siku hii ni manne, bora ni afuwatilize katika utaratibu ufuataao:

**1.** Kutupa vijiwe katika Jamratul A'qaba.
**2.** Kuchinja.
**3.** Kunyoa au kupunguza nywele.
**4.** Kutufu nyumba ya Allah na kufanya sa'ayi kwa mutamati', kadhalika aliyefanya hajji ya Qiraan au Ifraad ikiwa hakufanya sa'ayi katika twawaaful Quduum.

Na hata asipo fuatiliza utaratibu huu, hajji yake ni swahihi na hana kosa lolote. Inaingia katika hayo pia kutanguliza sa'ayi kabla ya twawaaf, kwani imethubutu kuwa Mtume ﷺ aliulizwa juu ya yule aliye tanguliza sa'ayi kabla ya twawaaf akajibu: "Haina neno" Imepokewa na Abuu Daawud.

Na kutapatikana kuhalalika kikamilifu kwa mambo matatu: (kutupa vijiwe, kunyoa au kupunguza, na twawaaful Ifaadha pamoja na sa'ayi) akifanya mambo haya matatu, ni halali kwake kila alicho haramishiwa kwa ihram, hata kumkaribia mke wake pia. Ama akifanya mawili katika haya, basi atahalalika na kila kitu alicho katazwa wakati wa ihram ila mke wake hataruhusiwa kumkaribia mpaka afanye yote matatu.

## Kutupa Vijiwe Katika Jamratul 'Aqaba Kubwa Siku Ya Idd

Katika siku ya Idd (yaumu Nnahri), hata tupa vijiwe isipokuwa katika Jamratul 'Aqaba kubwa, kwa namna ifuatavyo:

**1.** Anapofika Mina baada ya kutoka Muzdalifa, ataelekea kwenye Jamratul 'Aqaba kubwa, atakapofika atakata talbiya ili kujishughulisha na kutupa vijiwe.

**2.** Kisha atatupa vijiwe saba kwa kufuatana (kimoja baada ya kingine), na lau kama atatupa yote saba kwa pamoja basi itahesabika ni kama aliyetupa kijiwe kimoja, kwa hiyo ni lazima atupe moja baada ya jingine.

**3.** Kila anapotupa kijiwe atapiga takbira kwa kusema “Allahu Akbar”.

**4.** Ni lazima ahakikishe kila kijiwe kimeingia ndani ya shimo lililoko katika Jamratul ʽaqaba kubwa, kwani la muhimu ni kijiwe kuingia ndani ya shimo wala sio kupiga ukuta.

**5.** Wala sio Sunnah kusimama na kuomba dua baada ya kutupa vijiwe katika siku hii.

**6.** Wala asitumie vijiwe vilivyotumika, ingawa akitumia itamtosheleza, ila ni bora ajiepushe.

**7.** Vijiwe vinavyotumika ni kiasi cha konde ya tende au maharagwe, wala haijuzu kutupa vijiwe vikubwa, wala kutupa viatu na mfano wake.

**8**. Na wakati wa kutupa vijiwe katika Jamratul 'aqaba kubwa ni kuanzia nusu ya usiku wa kuamkia tarehe kumi (siku ya Idd), na pia aweza kutupa vijiwe baada ya adhuhuri mchana wa siku ya Idd, hata ikifikia usiku, kwa sababu hakuna dalili inayokataza kutupa vijiwe vya siku hiyo katika usiku wa kuamkia tarehe kumi na moja.

**9.** Ama kutupa vijiwe kabla ya adhuhuri katika masiku ya Tashriiq (tarehe 11, 12, na 13 ya dhul-hijja) HAIJUZU WALA HAITOSHELEZI, kwa sababu hakika Mtume ﷺ alitupa vijiwe katika masiku ya Tashriiq baada ya adhuhuri (zawaal), na pia maswahaba wake, na lau kama kungalikuwa na ruhusa angelibainisha Mtume ﷺ ruhusa hiyo, kwa sababu kusubiri mpaka wakati wa zawal kuna uzito, pamoja na uzito huo hakufanya yeye wala hakuwapa idhini walio madhaifu na mfano wao kutangulia kutupa vijiwe siku hizo, kama alivyowapa ruhusa kuondoka Muzdalifa mapema, na hii ni dalili ya wazi ya kuwa HAIJUZU WALA HAITOSHELEZI KUTUPA VIJIWE KABLA YA ZAWAL . Na hii ndio qauli ya Imam Malik, Abu Hanifa, Shafii na Ahmad na ndio qauli inayo ambatana na Sunna ya Mtume. ﷺ

**10.** Yajuzu kumuwakilisha mtu mwengine atupe vijiwe kwa niaba ya yule asie kuwa na uwezo wa kutupa vijiwe mwenyewe, kama mgonjwa au mtu mzima au kipofu ambao kwao wao ni uzito kwenda kutupa vijiwe wenyewe, watamtuma atakae wawakilisha katika jambo hilo, ama mwenye uwezo wa kufanya hivyo kwa nafsi yake, basi haijuzu kuwakilisha mtu amtupie, na lau kama atawakilisha mtu basi haitamtosheleza.

**11.** Na anayemuwakilisha mwengine katika kutupa vijiwe, mwanzo aanze na kujitupia vijiwe vyake, kabla ya kumtupia anayemuwakilisha, wala haijuzu kwa asiyekuwa katika matendo ya hajji kumwakilisha anayefanya hajji.

## Kuchinja Siku Ya Idd

Baada ya kutupa vijiwe siku ya kumi basi atafanya yafuatayo:
**1.** Atakuja sehemu ya kuchinja iliyoko Mina achinje wanyama wake, hivi ndivyo ilivyo Sunna, kutupa vijiwe kisha kuchinja ingawa si lazima.

**2.** Inajuzu kuchinja sehemu yoyote ya Mina na kadhalika Makka, lakini haijuzu kuchinja kichinjo hicho nje ya mipaka ya haram, na akifanya hivo basi kichinjo hicho hakitamtosheleza, na itambidi achinje tena ndani ya mipaka ya haram, kwa sababu Mtume ﷺ pamoja na maswahaba wake hawakuchinja isipokuwa ndani ya mipaka ya haram.

**3.** Na inajuzu kwa watu saba kushirikiana katika kuchinja ngamia mmoja au ng'ombe mmoja, na hiyo itawatosheleza.

**4.** Na asiyekuwa na uwezo wa kuchinja basi atafunga siku tatu katika hajji na siku saba atakaporudi kwao.

**5.** Ana uhuru katika kufunga kwake saum hiyo ya siku tatu, akitaka atafunga kabla ya siku ya Idd na akitaka atafunga masiku ya Tashriiq matatu (tarehe 11, 12 na 13).

**6.** Na ni bora Zaidi ikiwa atafunga siku tatu hizo iwe ni kabla ya siku ya Idd, na pia afunge kabla ya siku ya A'rafa, kwa sababu Mtume ﷺ alsimama A'rafa akiwa hakufunga na alikataza mahujaji kufunga siku ya A'rafa, kwa sababu ni uchangamfu kwake zaidi kumtaja Allaah na kuomba dua.

**7.** Na wakati wa kuchinja ni siku nne: siku ya Idd na masiku ya Tashriiq (11, 12 na 13).

## Kupunguza Nywele au Kunyoa (Kipara) Katika Siku Ya Idd

**1.** Ni Sunna iwe baada ya kutupa vijiwe na kuchinja, ingawa akitanguliza itajuzu.

**2.** Atanyoa kichwa chake chote (kipara) au atapunguza kichwa chake chote, wala haitoshelezi kupunguza baadhi ya sehemu za kichwa na kunyoa (kipara) ni bora Zaidi.

**3.** Na ikiwa mtu alipunguza baadhi ya sehemu za kichwa bila kujua hukmu yake basi itamtosheleza.

**4.** Na ni Sunna aanze kinyozi kunyoa upande wa kulia wa kichwa.

**5.** Ama kwa mwanamke atapunguza kadri ya ncha ya kidole baada ya kukusanya nywele zake pamoja.

## Twawaaful Ifadha

**1.** Nayo ni nguzo katika nguzo za hajji.
**2.** Haiswihi Twawaaf hii kabla ya mtu kusimama A'rafa.
**3.** Wakati wake unaanza baada ya nusu ya usiku wa kuamkia Idd baada ya kuondoka Muzdalifa.
**4.** Na ni Sunna kwa Twawaaf hii iwe baada ya kutupa vijiwe, kuchinja na kunyoa au kupunguza nywele, ingawa yajuzu kuitanguliza.

## Namna ya kuitekeleza twawaafu hii ni kama ifuatavyo:

**1.** Anapo halalika kuhalalika kwa kwanza (nako hupatikana kwa mtu: kutupa vijiwe na kunyoa au kupunguza nywele), atajitia manukato kisha atakwenda msikiti wa Makka kwa ajili ya kufanya twawaaf.

**2.** Atatufu mara saba, kwa namna tulivyo ieleza mwanzo, isipokuwa hata wacha bega lake nje wala hatatufu upesi katika mizunguko tatu ya mwanzo kama alivyo fanya katika twawaaful qudum.

**3.** Na ni katika Sunna kuswali rakaa mbili baada ya twawaaf kama tulivyo eleza mwanzo.

**4.** Baada ya hapo kwa mwenye kufanya hajji ya tamatu'u atafanya sa'ayi baina ya Swafaa na Marwa kwa namna tulivyo eleza mwanzo.

**5.** Kufikia hapa ni lazima ifahamike kuwa mwenye kufanya hajji ya tamatu'u, atafanya sa'ayi mara mbili: ya kwanza anapo fanya umra, na ya pili kwa ajili ya hajji yake, wala haimtoshelezi sa'ayi moja.

**6.** Baada ya twawaaf hii atakua amehalalika kikamilifu, na ni halali kwake kila kilicho haramishwa na ihram hata kumkaribia mkewe, na hii ndio inayo itwa kuhalalika kwa pili.

**7.** Baada ya hapo atakwenda kwenye maji ya zamzam na kunywa maji ya zamzam na kujimwagia kichwani.

**8.** Kwa mwanamke aliyepata ada ya mwezi kabla ya kutufu twawaaf hii, atasubiri pamoja na mahrim wake hadi atwahirike, ikiwa hakumakinika kuifanya twawaaf hiyo kwa kuhitajika kurudi nchi yake  kabla ya kutwahirika, atasafiri kwenda kwao baadae

arudi anapo twahirika ili kuitekeleza twawaaf hii, ama ikiwa ni mkaazi wa nchi za mbali hapo itajuzu kwake kuvaa kitakacho muhifadhi, kisha atatufu kwa nia ya Hajji na itamtosheleza, na hii ni kauli ya wanawavyuoni miongoni mwao:
Sheikhul Islaam Ibnu Taymiya, na Ibnul Qayyim na wengineo.

## Kulala Mina:

**1**. Baada ya kutufu twawaaful Ifadha, ataregea Mina abaki huko siku hiyo ya Idd na masiku ya Tashriiq, nazo ni siku tatu mchana na usiku, tarehe 11, 12 na 13.

**2.** Kulala Mina ni katika mambo ya wajib katika hajji.

**3.** Kinacho zingatiwa katika kulala Mina, ni kupitisha sehemu kubwa ya usiku sehemu hiyo, kwa sababu sheria haikuweka mipaka katika mda wa kulala Mina, kwa mfano usiku una masaa kumi, mtu kukaa masaa sita yatosheleza.

**4.** Hakuna kosa kwa yule aliye na uzito, akiwa atakaa mchana wake Makka na usiku arudi Mina, na ni bora zaidi kwake kukaa Mina usiku na mchana.

**5.** Na yajuzu kwake kuzuru al Kaaba na kutufu katika kila usiku wa Mina kwa sababu Mtume ﷺ alifanya hivyo.

**6**. Ni waajib kwa aliye katika ibada ya hajji kuswali swala zake zote tano kwa jama'a.

**7.** Na ni juu ya kila aliye katika ibada ya hajji kukithirisha kumtaja Allaah katika masiku haya machache.

## KUTUPA VIJIWE KATIKA VIKUTA MASIKU YA TASHRIIQ (TAREHE 11, 12 NA 13)

Navyo ni vikuta vitatu: kikuta kidogo, kikuta cha kati na kikuta kikubwa.
**1.** Atatupa vijiwe katika vikuta hivyo vitatu, kila siku katika masiku ya Tashriiq baada ya zawal (dhuhri), kwa vijiwe saba katika kila kikuta, na atafuata mpangilio kwa kuanza na kikuta kidogo kisha cha kati na mwisho kikubwa.

**2.** Ataanza na kikuta kidogo, anapomaliza kutupa vijiwe atasonga mbele kidogo upande wa kulia, atasimama akielekea qibla kisimamo kirefu akiomba dua, na atanyanyua mikono yake.

**3.** Baada ya hapo atakwenda katika kikuta cha kati atupe vijiwe kama alivyotupa katika kikuta kidogo, kisha ataenda upande wa kushoto, asimame kisimamo kirefu huku akielekea qibla, na kunyanyua mikono kuomba dua.

**4.** Baada ya hapo atakwenda katika kikuta kikubwa na kutupa vijiwe, Kaaba ikiwa upande wake wa kushoto na Mina upande wa kulia, anapomaliza kutupa vijiwe hapa, hata simama kuomba, bali ataondoka, na hii ndiyo Sunna.

**5.** Kisha atatupa vijiwe siku ya pili na ya tatu kwa namna tuliyo itaja.

**6.** Atatupa vijiwe akitaka katika sehemu ya juu, ya kati au ya chini, kama ilivyo jengwa karibuni.

## Kufanya haraka katika masiku ya Mina

Amesema Allah aliyetukuka:

"وَاذْكُرُوا اللَّهَ فِي أَيَّامٍ مَّعْدُودَاتٍ فَمَن تَعَجَّلَ فِي يَوْمَيْنِ فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ وَمَن تَأَخَّرَ
فَلَا إِثْمَ عَلَيْهِ لِمَنِ اتَّقَىٰ"

*"Na mtajeni Allaah katika zile siku zinazo hisabiwa.*
*Lakini mwenye kufanya haraka katika siku mbili (akarejea) si dhambi juu yake; na mwenye kukawia pia si dhambi juu yake, kwa mwenye kumcha Mungu."*

Na zile siku zinazo hisabiwa: ni siku za Tashriiq. Nazo ni siku tatu: siku ya kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu. Nayo ni masiku ya kula na kunywa na kumtaja kwa wingi Allah Subhaanahu wata'ala:

**1.** Anaye tupa vijiwe katika masiku ya kumi na moja na kumi na mbili, baada ya hapo akataka kufanya haraka kuondoka Mina basi itajuzu kwake kufanya hivyo bila matatizo, na atoke kabla ya kutua kwa jua la siku hiyo ya pili (siku ya kumi na mbili).

**2.** Na kwa yule atakae baki mpaka tarehe kumi na tatu ili atupe vijiwe siku hiyo, basi ni bora zaidi kwake, kwani ndivyo alivyo fanya Mtume ﷺ ,
pamoja na kuwa aliruhusu watu kuondoka tarehe kumi na mbili, ila yeye alibaki.

**3**. Lau kama atatupa vijiwe, na kuamua kuondoka tarehe kumi na mbili, jua likatua kabla hajaondoka, kwa ajili ya msongamano au sababu yeyote ile bila kukusudia, basi ataondoka na hana dhambi, kwa sababu kuchelewa kwake sio kwa khiyari yake.

**4.** Ama aliyebaki kwa khiyari yake mpaka jua likatua, hapo itamlazimu atimize na siku ya tatu (tarehe kumi na tatu).

## TWAWAAFUL WADAA'

**1.** Anapotaka aliyefanya hajji, kuondoka mji wa Makka, ni wajib kwake kutufu twawaaful Wadaa', hata kama ni kwa kubebwa ikiwa hawezi mwendo, liwe jambo la mwisho kwake ni kutufu twawaafu hiyo.

Ama watu wa Makka hawana Twawaaful Wadaa'.

**2.** Ama mwanamke aliye katika ada yake ya mwezi, huyu kwake sio wajib kutufu twawaaful Wadaa', kwa ruhusa waliyo pewa na Mtume ﷺ

**3.** Wala sio sawa kwa wanawake walio katika ada kusimama mlangoni mwa msikiti ili kuuaga msikiti, bali huu ni uzushi usokuwa na mashiko!

**4.** Atakapomaliza kutufu, atatoka na kutembea kama kawaida, kinyume na wanavyo fanya baadhi ya watu, ambao hutoka huku wakitembea kinyume, huu pia ni katika uzushi.

**5.** Baada ya twawaaf hii, asibaki Makka ila kwa ajili ya dharura, kama kukimiwa swala, kuswalia jeneza, au kununua zawadi akiwa njiani, ama kubaki bila ya dharura yoyote, itabidi aregelee tena twawaaful Wadaa'.

**6.** Twawaaful Wadaa' ni wajib kwa anaye hijji, wala sio wajib kwa anaye kwenda huko kwa ajili ya umra, bali hakuna dalili kuwa anaekwenda umra atakikana kufanya twawaaful Wadaa'.

Baada ya kufanya haya tuliyo yataja, hapo itakuwa yametimia matendo ya hajji.

Na Allaah ndie Mjuzi zaidi.

# ZIARA YA MASJIDI NABAWY NA ADABU ZAKE

**1.** Ni Sunna kuuzuru msikiti wa Mtume ﷺ katika wakati wowote, kwa waume na wake, na wala ziara hii HAINA MAFUNGAMANO YOYOTE NA HAJJI, sio katika masharti ya hajji, wala nguzo, wala wajibaat za hajji.

**2.** Anapowasili msikitini, anaezuru masjidi Nabawy, inapendekezwa atangulize mguu wake wa kulia wakati wa kuingia msikitini, na aseme dua ile ile kama anavyo sema anapoingia msikiti wowote mwengine, wala masjidi Nabawy hauna dua makhsusi tofauti na Misikiti mengine.

**3.** Akiingia ndani ataswali rakaa mbili, kama anavyo fanya akiingia msikiti wowote mwengine.

**4.** Akipata nafasi kuswali rakaa mbili katika Rawdha tukufu ni bora zaidi.

**5.** Baada ya hapo anaweza kwenda kuzuru kaburi la Mtume ﷺ na maswahaba wake wawili Abubakar na Omar radhi za Allaah ziwe juu yao.

**6.** Atasimama mbele ya kaburi la Mtume swallallaahu aleihi wa sallam, kwa adabu na kushusha sauti yake, kisha atamsalimia kwa kusema:

" اَلسَّلاَمُ عَلَيْكَ يَا رَسُوْلَ الله وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ "

**"Assalamu aleika yaa Rasuula llah warahmatullahi wabarakaatuhu"**

**7.** Baada ya kumsalimia Mtume ﷺ atamsalimia Abubakar na Omar – radhi za Allaah ziwe juu yao, kuwaombea, na kuwataradhia, kama alivyokuwa akifanya Abdullahi bin Omar:

" اَلسَّلاَمُ عَلَيْكَ يَا رَسُوْلَ الله،اَلسَّلاَمُ عَلَيْكَ يَا أَبَابَكَر،اَلسَّلاَمُ عَلَيْكَ يَا عُمَر "

**Assalamu aleika yaa Rasuula llah, assalamu aleika yaa Abaabakr, assalamu aleika yaa Omar.**

Baada ya kusalimia ataondaka.

**8.** Anapotaka kujiombea nafsi yake, ataelekea qibla wala sio kaburi, katika sehemu ya kando, aombe dua anayotaka.

**9.** Yapendekezwa kwa anaye zuru msikiti huu, aswali swala zake zote tano msikitini, ingawa hadithi ya kuswali swala arubaini kuna ajri kadhaa haikuthubutu!

*This book was pulished on*
*July 2019*
*(1440 Dhul Qai'da)*

# الحج والعمرة

